BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

OORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Kwanza – Tarehe 15 Mei, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 02 Machi, 2024.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2024/2025.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa Mwaka 2024/2025.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

116. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa kuwa kuna ongezeko kubwa la matukio ya moto katika majengo kama vile skuli, nyumba na masoko ambayo hupelekea hasara kubwa ya mali na hata kuweka hatarini uhai wa wananchi. Na kwa kuwa kazi ya kuzima moto iko chini ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar, ambacho kinakabiliwa na changamoto kubwa ya kukosa vifaa vya kisasa na mifumo imara ya kuzimia moto, kama vile pump maalum za mfumo wa maji zinazowekwa pembezoni mwa barabara (Fire Water Pumps House).

(a) Je, Serikali inalitambua tatizo hili na ni hatua gani huzichukua inapopanga mipango miji ili kuhakikisha kuwa mifumo hii inawekwa katika makaazi ya watu,

(b) Je, ni sehemu zipi kitaalamu zinapaswa kuwekewa mifumo hii ili kuwasaidia wazima moto kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

(c) Kwa kuwa kumekuwa na maboresho makubwa ya barabara nchini, Je, Serikali inazingatia vipi mahitaji ya mifumo hii.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

1. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kumekuwa na changamoto katika utozaji wa kodi ya miundombinu kwa watalii wanaolala katika hoteli za Zanzibar licha ya mifumo iliyopo ya ulipaji wa kodi kupitia Mamlaka za kukusanya kodi Zanzibar. Changamoto hii imeleta malalamiko makubwa kwa watalii wanaoingia na kutoka Zanzibar.

(a) Je, ni nani haswa anayepaswa kumtoza mgeni kodi ya miundombinu, na ni taratibu gani Serikali inazozisimamia ili kutatua suala hili.

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani madhubuti za kurekebisha mfumo wa kutoza kodi ya miundombinu ili kupunguza malalamiko ya watalii wanaolala katika hoteli za Zanzibar.

(c) Je, ni mikakati gani inayochukuliwa na Serikali kuhusu kutoza kodi ya miundombinu kwa watalii ili kuboresha uwazi na kuhakikisha kuwa kodi hizo zinatozwa kwa njia inayofaa kwa kuzingatia sheria za nchi.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

8. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika kujipatia ajira, wananchi wengi wa jimbo la Paje wanajiendeleza na kilimo cha ndimu, kama zao kuu la biashara.

(a) Je, Serikali ipo tayari kuwatafutia soko la nje ya nchi wakulima hao.

(b) Je, ni lini utawatembelea wakulima hao pamoja na kujionea wanavyolima zao hilo.

(c) Je, unawaambia nini wakulima wa jimbo la Paje kuhusu biashara ya zao la ndimu.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

9. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali imeamua kuwawezesha vijana kujiajiri kwa kuruhusu biashara ya boda boda kwa lengo la kujiajiri wenyewe. Pamoja na jambo hilo jema, kuna changamoto mbali mbali zinajitokeza.

(a) Je, hadi sasa kuna ajali ngapi zimejitokeza zilizosababishwa na usafiri wa boda boda.

(b) Je, vifo na majeruhi wangapi waliosababishwa na usafiri wa boda boda kwa mwaka 2023.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

2. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na utaratibu usio rasmi, unaogharimu na usiowafurahisha baadhi ya wananchi wa kuendesha kambi za kusomea maskulini hasa kwa madarasa yanayokabiliwa na mitihani ya Taifa, Serikali pamoja na kulifahamu kwake, bado haijalitolea kauli rasmi jambo hili.

(a) Je, ni jambo gani linalolazimisha maskuli kuweka kambi katika mazingira ambayo sio rasmi na rafiki kwa watoto.

(b) Je, Serikali haioni ulazima wa kuwa na mtaala unaoruhusu kusomeshwa na kudurusiwa ndani ya muda uliopangwa kwa madarasa yenye mitihani ya Taifa ili kuepusha ulazima wa kuweka kambi maskulini.

(c) Kama Serikali imehakikisha kwamba kambi ni njia bora ya kuongeza ufaulu na ufanisi wa wanafunzi na skuli, je, kwa nini haitengenezi utaratibu wa kuzirasimisha kambi katika maskuli kwa madarasa yenye mitihani ya Taifa.

89. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Moja ya kati ya mambo yaliyopelekea matokeo chanya kwa Wizara hii ni utoaji wa nauli kwa wafanyakazi wake ambao walikuwa wakitoka masafa ya mbali na vituo vyao vya kazi, kwa kuwa jambo hili lilionesha ufanisi tosha kwa Wizara.

Kwa nini Wizara imeamua kuondoa utamaduni huo ambao huwapunguzia dhiki watendaji wake hususani walimu.

**Wizara ya Afya:**

44. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa kumekuwa na tatizo kubwa la watoto kuzaliwa wakiwa na ugojwa, aidha wa tundu kwenye moyo, moyo mkubwa na mengine yaliyo na mnasaba na moyo. Na kwa kuwa tiba ya tatizo hilo inahitaji gharama kubwa sana ambapo wanachi wengi hushindwa kufidia matibabu hayo.

(a) Je, ni sababu gani hasa za kitaalamu zinazopelekea tatizo hili kwa watoto wachanga.

(b) Je, Wizara ina mpango gani katika kupunguza tatizo hilo.

(c) Je, Wizara imejipanga vipi kupitia Mfuko wa Bima ya Afya kukidhi gharama hizo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

5. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kuanzishwa kwa maktaba ya vitabu vya lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa ajenda muhimu ya Serikali yetu.

Je, tathmini iko vipi juu ya utekelezaji wa wazo hili.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2024/2025.

**Zanzibar,**
**15 Mei, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**